Jikinge, jilinde, Chukua Tahadhari

Juni

# TIRA Updates 2025

Kwa Soko Salama la Bima

Toleo No.07 | Jarida la Mtandaoni | www.tira.go.tz




HALIUZWI

## Bima ni Kinga, Bima ni Ngao, Bima ni Maendeleo

# Yaliyomo

Juni 2025

01




03





**Jarida Hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma**

**Mhariri**
Hadija Maulid

**Waandishi**
Tabia Mchakama
Anna Massao

**Msanifu**
Abubakari W. Kafumba



01 Simbachawene Atembelea Banda la Wizara ya Fedha Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma

02 TIRA Wapongezwa kwa Maendeleo Sekta ya Bima Nchini

03 Katibu Mkuu Utumishi Asisitiza Bima kwa Magari ya Serikali Wiki ya Utumishi wa Umma

04 Dkt. Saqware Azindua Bima Kidijitali kwa Vikundi, Suluhu la Bima Kiganjani

06 Bima Walk Yafana, Wadau wa Bima Washiriki Kuhamasisha Matumizi ya Bima

07 TIRA Kanda ya Magharibi Yakutana na Watoa Huduma za Bima

08 TIRA Kanda ya Kaskazini Yatolea Elimu ya Bima kwa Jukwaa la Maendeleo ya Ushirika

09 TIRA Unguja Yatoa Elimu ya Bima kwa Watumishi Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar

10 Tunarudisha kwa Jamii Wadau Sekta ya Bima Wachangia Madawati Shule ya Msingi Meru Arusha

12 TIRA Ndani ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2025 Dodoma


TIRA Updates ni jarida la mtandaoni linaloandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, likilenga kutoa taarifa muhimu, kuelimisha, na kuhamasisha umma kuhusu sekta ya bima nchini. Jarida hili limeandaliwa ili kufikia wadau mbalimbali wa sekta, wakiwemo mawakala wa bima, kampuni za bima, watoa huduma na watumiaji wa bima.

Jarida la TIRA Updates lina taarifa za matukio mbalimbali, ikijumuisha uzinduzi wa miradi mipya, semina, warsha za mafunzo, na mikutano muhimu inayofanyika ndani ya sekta ya bima.

Mbali na taarifa za matukio, TIRAUpdates lina makala maalumu zinazolenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima.

Aidha, toleo hili litaangazia matukio, habari na taarifa muhimu za mwezi Juni 2025.




Scan
Kusoma Kidijiti


Kwa mawasiliano zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe
**info@tira.go.tz**

Au
Piga simu bure **+255 222 132 537**

Tovuti yetu
**www.tira.go.tz**

# Simbachawene Atembelea Banda la Wizara ya Fedha Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma







Mhe. George B. Simbachawene (Mb), Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, alitembelea banda la Wizara ya Fedha katika Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2025, na kupokea maelezo kutoka kwa Taasisi mbalimbali, ikiwemo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA).

Waziri alisisitiza matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma bora na uwajibikaji kwa umma.

# TIRA Wapongezwa kwa Maendeleo Sekta ya Bima Nchini




Mkutano huo ulifanyika Juni 20, 2025, naulifunguliwa rasmi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi. Zena A. Said katika hoteli ya Gran Melia, Arusha ambapo aliipongeza TIRA kwa ufanisi katika utendaji wake na kufanikiwa kukuza sekta ya bima.

Pia alipongeza maandalizi mazuri yaliyofanyika kuelekea Mkutano huo kama Bima Sport Bonanza, Matembezi ya bima (Bima Walk), Bima Debate na Urudishaji kwa jamii CSR.

Kwa upande wake Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware alieleza mafanikio na mikakati katika sekta hiyo na kutoa rai kwa watoa huduma kuongeza ufanisi ili kuwafikia watanzania wengi zaidi kutumia bidhaa za bima.

Mkutano huo ulihudhuriwa na watendaji wakuu wa kampuni za bima, washauri wa bima, mawakala wa bima na wadau wengine katika sekta hiyo muhimu katika kukuza uchumi wa taifa letu.

# Katibu Mkuu Utumishi Asisitiza Bima kwa Magari ya Serikali Wiki ya Utumishi wa Umma




Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Juma Mkomi, alitembelea banda la Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) katika Maonesho ya Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2025 yaliyofanyika katika viwanja vya Chinangali Park, jijini Dodoma.

Bw. Mkomi alisisitiza umuhimu wa uchapakazi na uwajibikaji kwa watumishi wa umma ili kuongeza weledi na ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Aidha, akiwa katika banda la TIRA, alieleza umuhimu wa magari ya Serikali kukatiwa bima ili kuhakikisha yanakuwa na kinga dhidi ya majanga, jambo litakalosaidia kuipunguzia Serikali hasara iwapo ajali au madhara yatatokea.

Kwa sasa, TIRA inaendelea kuishauri Serikali umuhimu wa kukatia bima magari yake yote kama sehemu ya usimamizi wa rasilimali na ulinzi wa mali za umma.

# Dkt. Saqware Azindua Bima Kidijitali kwa Vikundi, Suluhu la Bima Kiganjani





Katika hatua ya kuimarishaupatikanaji wa huduma za bima kwa wananchi wa kawaida, Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware alizindua rasmi Kampeni mpya ya Bima ya Vikundi Kidijitali jijini Dar es Salaam.

Kampeni hii ililenga kuwafikia Watanzania walio kwenye vyama na vikundi vya kijamii vya kuweka na kukopa kwa kutumia teknolojia rahisi inayopatikana kupitia simu za mkononi.

Akizungumza katika hafla hiyo ya uzinduzi, Dkt. Saqware, alipongeza ubunifu ulioonyeshwa na Benki ya NMB kwa kushirikiana na Kampuni ya Bima ya MetroLife katika kuleta huduma ya bima iliyo rahisi, ya kidijitali na inayolenga wananchi wa kawaida.

Alieleza kuwa mpango huu mpya unaendana kikamilifu na malengo ya Serikali ya kuongeza idadi ya wananchi walioko kwenye mifumo rasmi ya bima, hatua ambayo itasaidia kupunguza utegemezi wa kifamilia na kijamii pindi majanga yanapotokea. "Ubunifu huu wa Bima ya Vikundi kupitia simu ni suluhisho kwa changamoto ya upatikanaji wa bima kwa wananchi wengi. Ni wakati sasa kwa taasisi za kifedha




kuendelea kushirikiana na sekta ya bima kuifikisha huduma hii kwa watu wengi zaidi, hasa walioko kwenye vikundi," alisema Dkt. Saqware.

Kwa upande wake, Afisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara kutoka Benki ya NMB, Bw. Filbert Mponzi, alifafanua kuwa huduma hiyo mpya ya Bima ya Vikundi imebuniwa mahsusi kwa ajili ya kusaidia wanavikundi kushiriki kwa kuchangia kiwango kidogo kuanzia Shilingi 500, lakini kinachopatikana kwa wanufaika ni kikubwa. "Kwa mfano, mwanachama wa kikundi akifikwa na msiba, anaweza kupata mkono wa pole hadi kufikia Shilingi Milioni Moja kupitia bima hii.

Na sasa huduma hii inapatikana hata kupitia wakala wa NMB Jirani, hivyo hakuna haja ya kwenda matawini," alisema Bw. Mponzi.

Alitoa wito kwa wananchi kujiunga na huduma hiyo kwa kufungua akaunti za benki kupitia simu na kujiunga na vikundi vilivyosajiliwa, akisisitiza kuwa huduma hiyo tayari imeanza rasmi na inapatikana nchi nzima kupitia mtandao wa NMB na MetroLife.

Kwa pamoja, NMB na MetroLife wameonesha njia ya jinsi ubunifu wa kidijitali unavyoweza kufungua milango ya fursa kwa wananchi, hasa wale waliokuwa mbali na huduma za kifedha na bima. Uzinduzi huu unatarajiwa kuwa chachu ya mabadiliko katika mwitikio wa wananchi kuelekea huduma za bima.

# Bima Walk Yafana, Wadau wa Bima Washiriki Kuhamasisha Matumizi ya Bima



Matembezi ya kilometa tano za ushindi yalifanywa kwa moyo wa uhamasishaji lengo likiwa ni kuhamasisha matumizi ya bima nchini ambapo kwa mwaka huu ilikuwa zamu ya Arusha.

Matembezi hayo yalifanywa na wadau mbalimbali wa bima tarehe 19 Juni 2025 na yalianza rasmi katika viwanja vya Mgambo, Arusha na kumalizikia eneo hilo pia.

Akitoa pongezi na shukrani Mkuu wa Wilaya Arusha Bw. Joseph Mkude, kama Mgeni Rasmi wa tukio hilo aliwapongeza wadau walioshiriki na Kamati kulichagua jiji hilo la kitalii kuhamasisha matumizi ya bima. Pia Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mawaziri Mhe. Mhandisi Zena Said aliungana na wadau kushiriki matembezi hayo kama Mgeni maalumu.

Aidha, Bi. Hawa Mniga Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala kwa Niaba ya Kamishna wa Bima aliwapongeza washiriki wote na kusema matembezi hayo yameongeza chachu na ari katika matumizi ya bima jijini humo na jamii nzima kwa ujumla.

Matembezi hayo yalikuwa sehemu kuelekea Siku ya Bima Tanzania yaliyofanyika tarehe 20 Juni 2025.

# TIRA Kanda ya Magharibi Yakutana na Watoa Huduma za Bima




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kanda ya Magharibi inayohudumu mikoa ya Tabora, Shinyanga na Singida ilikutana na watoa huduma za bima wa kanda hiyo tarehe 03 Juni 2025 katika ofisi za Mamlaka mkoani Tabora. Lengo likiwa kukumbushana masuala mbalimbali katika sekta ya bima.

Meneja wa Kanda hiyo Dkt. Emmanuel Lupilya wakati wa ufunguzi wa mkutano huo alieleza lengo la kukutana ni kukumbushana uwajibikaji na ufanisi katika utoaji huduma, umuhimu wa uandikishaji biashara, uzingatiaji wa miongozo, matumizi ya mabango sahihi yaliyowekwa na Mamlaka lakini pia kuongeza fursa na uandikishaji wa bima.

Vilevile, Meneja Lupilya pia alisisitiza juu ya umoja kwa wasajiliwa hao kama chanzo cha ukuzaji wa huduma na pia kueleza ushirikishwaji wa wadau hao katika utoaji elimu ya bima ili kuongeza uelewa na matumizi ya bima nchini.

Ofisi za TIRA mkoani Tabora zipo TUWASA Barabara ya boma, mtaa wa Gongoni mkoani Tabora.

# TIRA Kanda ya Kaskazini Yatolea Elimu ya Bima kwenye Jukwaa la Maendeleo ya Ushirika




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia ofisi zake za Kanda ya Kaskazini ilitoa elimu ya bima kwa viongozi na wanachama wa vyama vya ushirika wa mkoa wa Kilimanjaro, Arusha na Tanga katika Maonesho ya Vyama vya Ushirika yaliyofanyika kuanzia Mei 30 – Juni 5, 2025.

Jumla ya wananchi 1,037 walipewa elimu ya bima katika maonesho hayo matatu ikiwa ni pamoja na vyama vya kukopesha (SACCOS), vyama vya wakulima (AMCOS) na vyama mbalimbali vya ushirika, taasisi za serikali na mashirika ya umma ikiwemo taasisi ya kupambana na rushwa (PCCB), Chuo cha ushirika na Benki ya Ushirika pamoja na wadau wa bima.

Meneja wa Kanda hiyo Bw. Bahati Ogolla akiongea na TIRA Updates alieleza lengo la kushiriki Maonesho hayo ni kufikia lengo la asilimia 80 ya wananchi wanafahamu masuala ya bima ifikapo mwaka 2030 kama ambavyo imebainishwa kwenye Mpango Mkuu wa Maendeleo wa Sekta ya Fedha wa miaka kumi (2020/2021 – 2029/2030) lakini pia kusikiliza malalamiko na maoni mbalimbali kutoka kwa wananchi.

# TIRA Unguja Yatoa Elimu ya Bima kwa Watumishi Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar




TIRA, Kanda ya Unguja, Zanzibar Juni 12, 2025 ilitoa semina ya elimu ya bima kwa watumishi wa Wizara ya Biashara na Viwanda ikiwa ni muendelezo wa matukio mbalimbali ya utoaji elimu kukuza uelewa na matumizi ya bima visiwani humo.

Semina hiyo pia ilihusisha mijadala ya maswali na majibu yaliyojibiwa kikamilifu kutoka Mamlaka. Meneja wa Kanda hiyo Bi. Awanje Matenda alieleza TIRA Updates lengo la kanda hiyo ni kuona matumizi ya bima yanaongezeka kila mwaka na wananchi wanaweza kujikinga na majanga.

Watumishi wapatao hamsini (50) walinufaika na elimu hiyo.

Visiwani Zanzibar zipo ofisi mbili za Kanda za Mamlaka ambazo zipo Unguja na Chakechake Pemba.

Pamoja na majukumu ya utoaji elimu lakini pia hufanya jukumu la kusajili na kutoa leseni kwa watoa huduma za bima na shughuli nyingine mbalimbali ndani ya sekta ya bima.

# Tunarudisha kwa Jamii; Wadau Sekta ya Bima Wachangia Madawati Shule ya Msingi Meru Arusha



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kwa kushirikiana na Taasisi ya Bima Tanzania (IIT) pamoja na wadau wengine kama Kampuni za Bima Juni 18, 2025 walifanya tukio la urudishaji kwa jamii (CSR) kwa kuchangia madawati katika shule ya Msingi Meru iliyopo Halmashauri ya Jiji la Arusha tukio lililoenda sambamba na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Siku ya Bima Tanzania uliofanyika Juni 20, 2025.

Awali, wadau hao wa bima walikutana na Mkuu wa Wilaya, Halmashauri ya Jiji hilo Bw. Joseph Mkude ambaye alishukuru kwa msaada huo wa madawati na kuahidi kuendeleza ushirikiano na sekta ya bima.

Aidha, katika tukio hilo Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo Bw. Ibrahim Ndee aliishukuru TIRA na wadau hao wa bima kwakuwa madawati hayo yatasaidia kupunguza adha ya watoto kusongamana. Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Siku ya Bima Tanzania, Bw. Jared Awando aliwaasa wadau wa bima kuendeleza umoja na kurudisha kwa jamii ili kukuza sekta mbalimbali.

Pia Meneja wa TIRA Kanda ya Kaskazini Bw. Bahati Ogolla alimwakilisha Kamishna wa Bima Tanzania na kueleza Mamlaka kama wadau wa elimu wamekuwa wakitoa misaada mbalimbali kwa jamii kukuza sekta hiyo nchini.





# TIRA Ndani ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2025 Dodoma




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ilishiriki kwenye maonesho ya Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2025 yaliyofanyika Chinangali Park, Dodoma.

Maonesho hayo yalidumu kwa wiki moja, kuanzia tarehe 16 hadi 23 Juni 2025, yakiwa na kaulimbiu isemayo “Himiza matumizi ya mifumo ya kidijiti ili kuongeza upatikanaji wa taarifa na kuchagiza uwajibikaji”.

Wananchi walipata fursa ya kujifunza kuhusu huduma mbalimbali za bima, haki na wajibu wa mteja wa bima.


are you covered?


WIZARA YA FEDHA

# Majibu ya Maswali yako Kuhusu Bima

*Pata majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara*



## Bima ni nini?

Bima ni mkataba wa kisheria kati ya pande mbili yaani kampuni ya bima na mtu binafsi, kikundi au kampuni (mbima), ambapo kampuni ya bima inaahidi kulipa fidia iwapo janga lililokatiwa bima litatokea na kusababisha hasara. Hivyo, bima ni nia ya kuhamishia majanga kwa kampuni za bima na kupata kinga dhidi ya majanga mbalimbali yasiyotarajiwa. Bima hukatwa kwa ajili ya kukinga majanga mbalimbali yanayotuzunguka kila siku.

## Majanga ni nini?

Ni hatari yeyote isiyotabirika inayoweza kusababisha upotevu wa fedha, maisha na mali. Hatari hizi zinaweza kutokea katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na za kijamii kila siku. Hivyo, matukio kama ajali za vyombo vya usafiri, moto, mafuriko, magonjwa, ukame ni baadhi tu ya majanga yanayoweza kumkumba mwananchi.

## Bima ina umuhimu gani kwa mali na maisha ya mwananchi?

Bima ni muhimu kwani inahakikisha usalama wa kukabiliana na aina yoyote ya changamoto maishani. Bima ni sehemu muhimu sana katika mipango ya mwananchi katika uwekezaji wa kiuchumi na kijamii.

## Je, ni nani anastahili kuwa na Bima?

Bima ni nyenzo muhimu sana kwa kila mwananchi, hivyo hakuna anayebaguliwa ama kupewa kipaumbele sana katika kupata huduma za bima.

Hii ni kwa sababu kila mmoja kwa wakati fulani hukumbwa na janga aidha la kiuchumi (kupata hasara katika Biashara, kilimo, ufugaji n.k) na kijamii (yaani kuuguliwa, kufiwa na hata watoto kukosa ada na chakula n.k). Hivyo, kuzingatia aina hii ya uwezekano wa kupatwa majanga, jamii yote huhitaji bima za aina mbalimbali kulingana na uhitaji.

## Ni nani aliyepewa dhamana ya kutoa huduma za Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, Soko la Bima nchini linasimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ambayo hutoa leseni kwa kampuni za bima ambazo hubeba dhamana ya kutoa fidia kwa wananchi waliokata bima.

Pia, wananchi wanaweza kupata huduma za bima kupitia Washauri na Madalali wa Bima, Mawakala wa Bima kupitia Benki na Mawakala wa Bima waliosajiliwa na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria. Pia, kuna watoa huduma za bima wanaosajiliwa na Mamlaka kama Wakadiria Hasara, Wakaguzi Binafsi na Wakala wa Ufuatiliaji wa Fidia.

## Ni wakati gani Bima inahitajika?

Bima inahitajika mara tu unapokuwa hauna uhakika na uwezekano wa kuwa katika hali yako ya awali iwapo janga litakupata. Hivyo, ni vema ikafahamika kuwa bima hukatwa mapema ili kujikinga na janga kabla halijatokea. Iwapo itakatwa baada ya janga kutokea haitofaa kutoa fidia kwa janga lililopita.

## Je, ni lazima kuwa na Bima?

Kimsingi, mwananchi anawajibika kukinga mali na wapendwa wake kwa hiari yake kwa kuwakatia bima. Pamoja na hiari hiyo, Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168 ya Mwaka 1973, iliyorekebishwa 2002 imewapasa wamiliki wa vombo vya moto wanaotumia barabara za umma kukata bima ndogo (Third Party Insurance) ili kumkinga mtu wa tatu dhidi ya majanga yanayosababishwa na vyombo vya moto.

## Je, ni nani mnufaika wa Bima?

Bima hunufaisha wamiliki wa bima au wakata (policyholders) na wahanga kulingana na aina

ya bima iliyokatwa na majanga yaliyosababisha hasara. Kwa mfano, Bima za Maisha na Bima za Afya hunufaisha mkataji bima ama wanufaika walioandikwa katika mkataba wa bima.

Kwa upande wa Bima za Muda Mfupi, mnufaika wa kwanza huwa ni mkata bima hususan kwenye bima za moto, kilimo, ajali, biashara, n.k. Bima ndogo (Third Party) hunufaisha moja kwa moja mtu wa tatu aliyesababishiwa janga iwe kuumizwa yeye mwenyewe ama kuharibiwa mali zake.

## Mkata bima ana wajibu katika suala zima la kupata huduma za Bima?

Ni kweli kuwa mkata bima anao wajibu katika hatua za kukata bima na wakati bima iko hai.

Wakati wa kukata bima atawaibika kutoa taarifa zote zinazohitajika kwa ukweli usiyo na shaka (bila kuongopa), kujaza fomu ya uhitaji wa bima na kutaja wanufaika (hii ni kwa Bima za Maisha na Bima za Afya), kuwa na nyaraka zote muhimu wakati wa ukataji bima kabla ya kuchukua mkataba wa bima; kufanya madai kwa mujibu wa masharti ya mkataba wa bima na kufuata mchakato wa madai.

## Je, pindi mkata bima anapopatwa na janga, ni wapi anatakiwa kutoa taarifa?

Pindi janga lililokatiwa bima linapotokea mkata bima mwenye mkataba wa bima anapaswa kutoa taarifa kwa kampuni ya bima iliyotoa kinga dhidi ya mali yake ili kuwezesha hatua zingine za fidia kuendelea. Utaoaji wa taarifa uzingatie taratibu zilizowekwa katika mkataba wa bima. Inashauriwa kutoa taarifa ndani ya masaa 24 baada ya janga kutokea.

Mhanga anaweza pia kutoa taarifa kwa wakala au dalali wa bima aliyemkatia bima. Lakini isisahaulike kuwa ni muhimu kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama na ngazi mbalimbali za Serikali, kwa mfano: inapotokea ajali, mkata bima atoe taarifa Jeshi la Polisi - Usalama Barabarani au nyumba inapoungua ni vema kutoa taarifa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji, kwa upande mwingine kuna Ofisi za Serikali za Mitaa, Vijiji na hata Kata.

Kutoa taarifa sehemu zote hizi hujenga msingi mzuri wa mkata bima kufidiwa bila mashaka ya tukio kwani linakuwa limehakikiwa na ngazi husika.

## Ni muda gani umewekwa kwa kampuni kushughulikia fidia kwa mhanga wa ajali au kuharibikiwa na mali iliyowekewa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, kampuni ya bima inapaswa kushughulikia madai ya wateja kwa muda mfupi kulingana na ukubwa wa janga na uthibitisho wa janga lenyewe kuwa halali. Baada ya kujiridhisha kuwa janga hilo ni sahihi na kutoa hati ya kukubali janga, kampuni itawajibika kutoa fidia kwa mteja ndani ya siku zisizozidi 45.

## Ni jinsi gani mteja anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ndicho chombo cha Serikali kinachowajibika kumlinda mteja wa bima (mkata bima). Hivyo, ni sahihi kabisa

kwa mnufaika wa huduma za bima kuleta lalamiko lake dhidi ya huduma za bima anazopewa na kampuni za bima zilizosajiliwa na Mamlaka. Malalamiko yanaweza kuwasilishwa TIRA kupitia barua pepe au simu, kutegemea uko eneo gani nchini. Pia unaweza kuwasilisha malalamiko kupitia tovuti: www.tira.go.tz ambapo utajaza fomu ya malalamiko na kuiwasilisha.

## Je, kuna tofauti kati malalamiko ya Bima na migogoro ya Bima?

Malalamiko ya bima ni tofauti kigodo na migogoro ya bima, kwani malalaiko ya bima hutokana na huduma hafifu zinazotolewa na watoa huduma wa bima kwa wananchi waliosajiliwa na Mamlaka na mara nyingi aina hii ya malalamiko uhusisha wahanga wa ajali (third party) na haya huwasilishwa kwa Kamishna wa Bima kwa hatua stahiki.

Migogoro ya bima ni ile inayohusisha mteja kutokubaliana na kiwango cha fidia kutoka kwa kampuni ya bima. Migogoro hii hupelekwa kwenye Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima Tanzania (TIO) kwa hatua zaidi.

## Je, kuna Bima kwa ajili ya kilimo na mifugo?

Soko la Bima nchini linaendelea kukua kila siku. Aina mbalimbali za bima zinatolewa ikiwemo Bima za Kilimo naBima za Mifugo. Bima ya Kilimo hukatwa kwa ajili ya kukinga moto, mafuriko, ukame, wanyama na wadudu waharibifu. Kwa upande wa Bima ya Mifugo, hutolewa kwa ajili ya kukinga magonjwa, upotevu na vifo.

## Je, TIRA ina mifumo yoyote ambayo inaitumia katika usimamizi wa shughuli za Bima kwenye soko?

Ndiyo. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ina mifumo mingi katika utoaji wa huduma za bima: Mafno: Mfumo wa TIRA-MIS unaotumika kukata bima na kuhakiki uhalali wa bima za vyombo vya moto na mali za mteja, mfumo mwingine ni Tanzania Import Insurance Portal (TIP) kwa ajili ya bima za mizigo kutoka nje ya nchi kwa njia meli (bahari) na dege (anga).

Pia mfumo wa Risk Based Supervision (RBS) kwa ajili ya upokeaji wa taarifa na uchambuzi wa viashiria vya majanga. Mifumo hii yote imeunganishwa na taasisi stahiki za Serikali pamoja na watoa huduma za bima.

## Je, ninaweza kuhakiki bima ya chombo cha moto na mali zangu?

Ndio, unaweza kuhakiki bima yako kwa kutumia mfumo wa TIRA-MIS.

## Je, Kuna Bima kwa ajili watu wa kipato cha chini?

Ndio. Ipo bima kwa ajili ya watu wa kipato cha chini, bima hii hufahamika kama "'microinsurance'. Ni bima ndogo ambayo ni kwa ajili ya kumkinga mtu asiyeweza kuingia kwenye utaratibu wa bima yenye gharama kubwa kutokana na kiwango cha fedha anachokipata.

Mfano kwa wale wanaofanya shughuli za uJuninga, mama/baba lishe, na wengine wenye biashara ndogo ndogo. Bima hizi hulipa fidia endapo mbima atapata hasara kwenye biashara yake aliyoikatia bima.



# TIRA & 2025


**Mamlaka ya Usimamizi wa Bima**
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
PSSSF HOUSE, 5th Floor, Makole Street, P.O. Box 2987
DODOMA, Tanzania.

coi@tira.go.tz
+255 26 2321180
+255 0222135137
+255 26 2321180

**FB, IG, X:** //@tira_tz
www.tira.go.tz